

# Kituo cha Msaada wa Majanga cha FEMA Kinafunguliwa katika Kaunti ya Windsor

---

**Release Date: Agosti 4, 2023**

Kituo cha Msaada wa Majanga kitafunguliwa Springfield Agosti 4 kusaidia wakaazi wa Vermont walioathiriwa na mafuriko kuanza kurudia hali ya kawaida. DRC ya pamoja, kituo cha muda kilichoanzishwa kwa ushirikiano kati ya Springfield, jimbo la Vermont na FEMA, itasaidia waathiriwa kutuma maombi ya msaada wa FEMA, kupakia hati na kujibu maswali ana kwa ana.

## **Kituo cha Springfield kinapatikana katika:**

Springfield Health Center  
100 River Street  
Springfield, VT 05156

## **Vituo tayari vimefunguliwa katika:**

Waterbury Armory  
294 Armory Drive  
Waterbury, VT 05676

ASA Bloomer Building  
88 Merchants Row, Suite 330  
Rutland, VT 05701

Barre Auditorium  
16 Auditorium Hill  
Barre, VT 05641

Flood Brook School  
91 VT-11  
Londonderry, VT 05148



**FEMA**

Page 1 of 2

Twinfield Union School  
106 Nasmith Brook Road  
Plainfield, VT 05667

Barton Memorial Building  
17 Village Square  
Barton, VT 05822

**Vituo vyote vinafunguliwa siku 7 kwa wiki, saa mbili asubuhi (8 a.m) hadi saa moja jioni (7 p.m.)**

Vituo vyote vinaweza kufikiwa na watu wenye ulemavu na mahitaji ya kutenda, na vina vifaa vya teknolojia ya usaidizi. Ikiwa unahitaji makao ya kuridhisha au mkalimani wa lugha ya ishara, tafadhali piga simu kwa 1-833-285-7448 (bonyeza 2 kwa Kihispania).

Wawakilishi kutoka Usimamizi wa Biashara Ndogo za Marekani (SBA) pia watakuwa kituoni kueleza jinsi ya kutuma maombi ya mikopo ya majanga yenye riba nafuu ya SBA kwa wamiliki wa nyumba, wapangaji, biashara na mashirika yasiyo ya kibiashara ya kibinafsi, na kutoa maelezo kuhusu kujenga upya ili kufanya nyumba zistahimili majanga zaidi.

Huhitaji kutembelea DRC ili kutuma maombi ya msaada wa FEMA. Kutuma ombi bila kutembelea kituo, piga simu kwa nambari ya msaada ya FEMA kwa **800-621-3362**, nenda mtandaoni kwenye [DisasterAssistance.gov](https://www.disasterassistance.gov) au upakue [FEMA App](#). Ikiwa unatumia huduma ya usambazaji kama vile huduma ya usambazaji video (VRS), huduma ya simu iliyo na maelezo mafupi au nyinginezo, pea FEMA nambari yako ya huduma hiyo unapotuma ombi.

FEMA imejitolea kuhakikisha msaada wa majanga unatekelezwa kwa usawa, bila ubaguzi kwa misingi ya rangi, dini, utaifa, jinsia, umri, ulemavu, ujuzi wa Kiingereza au hali ya kiuchumi. Mwathiriwa yeyote wa majanga au mwananchi anaweza kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Kiraia ya FEMA ikiwa anahisi kuwa ameathiriwa na ubaguzi. Ofisi ya Haki za Kiraia ya FEMA inaweza kupatikana bila malipo kwa 833-285-7448. Maopareta wa lugha mbali mbali wanapatikana.



**FEMA**

Page 2 of 2